

Je, Uko Tayari kwa Mahojiano Yako ya SNAP?

Wakati wa kuomba usaidizi wa Mpango wa Msaada wa Lishe ya Ziada (Supplemental Nutrition Assistance Program (SNAP)), katika hali nyingi mahojiano lazima yafanywe na mtaalamu wa msaada wa mpango (benefit program specialist (BPS)). Mahojiano haya ni taswira ya hali ya familia yako ili kubaini ustahiki wa usaidizi wa SNAP. Tunahitaji usaidizi wako kufafanua taarifa iliyio kwenye ombi lako la SNAP. Fikiria mahojiano haya kama mazungumzo ya binafsi kati yako na BPS kuhusu hali ya familia yako. Lengo la mahojiano ni kuweka kumbukumbu wazi ya hali yako, ili ombi lako la SNAP liweze kushughulikiwa bila kuchelewa.

Je, mahojiano haya yatafanyika wapi?

Mahojiano yanaweza kufanyika kuitia simu au ana kwa ana na mfanyakazi wa huduma za jamii kutoka idara ya eneo lako. Shirika la eneo lako litapanga miadi na kukutumia barua iliyio na maelezo ya miadi, kama vile tarehe na wakati.

Je, ni maswali gani yataulizwa wakati wa mahojiano ya SNAP?

Unaweza kutarajia kujibu maswali yaliyo kwenye ombi lako la SNAP, kama vile:

- Jina lako kamili na siku ya kuzaliwa ni gani?
- Nambari yako ya Ustawi wa Jamii ni gani?
- Unaishi wapi? (Unaweza kustahiki ikiwa huna nyumba au unaishi na familia/marafiki.)
- Je, wewe ni raia wa Marekani? (Watu wasio raia bado wanaweza kustahiki.)
- Mapato yako ya kila mwezi ni kiasi gani?
- Una akaunti ya benki ya aina yoyote?
- Unatumia huduma za kupasha joto au kupoza nyumba yako, na unalipa bili kwa ajili ya yoyote kati ya huduma hizi?
- Unalipa kodi au rehani au kulipia huduma za nyumbani kama vile umeme, gesi, maji au simu?
- Unalipa gharama ya kituo cha kutunza watoto mchana?
- Unalipa gharama za matibabu?

Je, ninahitaji kuwa na nini kwa mahojiano ya SNAP?

Unaweza kuwa na hati hizi ambazo zitakusaidia kujibu maswali kwa urahisi na kwa usahihi:

- Kadi ya Ustawi wa Jamii ikiwa huwezi kukumbuka namba yako.
- Stakabadhi za mshahara, barua za kukabidhiwa msaada (kama kutoka kwa Ustawi wa Jamii au Mamlaka ya Wanajeshi Waliostaafu), taarifa za pensheni, rekodi za kujijiri, rekodi za malipo ya malezi ya watoto, nk.
- Mkataba wa kukodisha, taarifa ya rehani au risiti ya kodi ya nyumba.
- Taarifa ya benki kwa akaunti za matumizi, kuweka akiba na chama cha mikopo.
- Bili za matumizi ya gesi, umeme au maji.
- Uthibitisho wa utambulisho. Hati hizi zinaweza kujumuisha:
 - Cheti cha kuzaliwa.
 - Leseni ya udereva.
 - Kadi ya Ustawi wa Jamii.

- Pasipoti.
- Visa ya kazi.
- Kadi ya mgeni mkazi.
- Stakabadhi ya mshahara.

Je, ninawezaje kujandaa kwa mahojiano yangu ya SNAP?

- Jitayarische kujibu tena, maswali yote yaliyo kwenye ombi la SNAP. Mhoji atakuwa akirekodi taarifa zako kwenye mfumo wa VDSS, ikiwa ni pamoja na maswali ambayo huenda umekosa kujibu au kujibu visivyo kwenye ombi.
- Jitayarische kutoa uthibitisho wa mapato, rasilimali na gharama ulizoripoti kwenye ombi lako. Mhoji atakujulisha hati unazohitaji kutoa wakati wa mahojiano na kukujulisha kwa maandishi.
- Jitayarische kujibu maswali yote yaliyo kwenye ombi la SNAP kwa kila mtu katika familia yako. Mahojiano hubaini usaidizi wako kwa kila mtu katika familia yako inayopokea SNAP.
- Jitayarische kujibu maswali kuhusu watu wengine wanaoishi nyumbani kwako ambaao hawaombi msaada wa SNAP.

Tumia msimbo wa QR kupata maelezo zaidi kuhusu mahojiano ya SNAP.

Nembo ya VDSS